

OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA HUDUMA INAZOHUSIANA NA WAKALA WA MELI.

ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0009

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza maandalizi ya awali ya ujenzi wa gati na kituo cha Upakiaji wa mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utooji wa huduma za:

Wakala wa meli na huduma zinazohusiana na meli za mizigo na vifaa vya shughuli za baharini

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shiriki la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelejaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalopita Uganda na Tanzania ikijumuisha gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, Tanga nchini Tanzania.

MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA: Majukumu ya Mawakala wa Usafirishaji ni pamoja na :

- Kuhakikisha nafasi kwa meli inayoingia bandarini,
- Kumsaidia kupata boti za kuongoza na kuvuta meli, kukiwa na uhitaji,
- Kuhakikisha upatikanaji wa vibali vya forodha na huduma za bandari,
- Kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa mabaharia

(maji safi, malazi, viburudisho, usafiri na vibali, viza, matibabu, n.k.).

- Kusaidia na kurahisisha mawasiliano na mamlaka kwa wakati.

KIWANGO CHA MAHITAJI:

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha vitu vifuatavyo:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifchedha na rasilimali za kutosha na zenyewe uwezo kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya uzoefu iliyօ na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika utekelejaji wa huduma za Kibali cha forodha, usafiri na huduma zinazohusiana na meli za mizigo na vifaa vya shughuli za baharini kulingana na viwango vya kimataifa katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linaloshabihiana
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipanga ya afya na usalama eneo la kazi na uthibitisho wa: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11, au yeti sawa;
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiva ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa Procurement@bbnjv.com. (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya **14 Oktober 2022**, saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo hapo juu yataathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

Kumbuka: Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeza mchakato wa Wito wa Zabuni.